

Dickson anaenda safari

Swahili

Dickson ni mtoto mdogo mwenye miaka mitano. Leo Dickson ataenda safari kutembelea wanyama kwa mara ya kwanza maishani mwake. Ataenda pamoja na mama na baba na dada yake Lulu mwenye miaka saba.

Mama yake aliamka mapema asubuhi kuandaa chakula kwaajili ya safari na alifungasha pia maji ya kunywa. "Siku ya leo itakuwa na joto sana kwahiyo itabidi tunywe maji mengi sana", alisema mama.

Baada ya kunywa chai ya asubuhi gari kubwa lilikuja kuwachukua. Dereva alikuwa anaitwa Frank na alikuwa ni rafiki wa baba. "Frank anajua kila kitu kuhusu wanyama wa porini", alisema baba.

Wote walipanda gari na kuelekea kwenye safari. Kabla ya kufika kwa wanyama dereva Frank alisimamisha gari na kufungua paa la gari ili wote waweze kusimama na kuona nje. "Vizuri sana. Sasa tutawaona wanyama kwa urahisi" alisema Dickson.

Mnyama wa kwanza kuonekana alikuwa ni tembo. Tembo alikuwa ni mkubwa sana na Dickson aliogopa kidogo mpaka ilimbidi amshike baba yake mkono. Tembo alikuwa na masikio makubwa sana na mkonge mrefu.

Mnyama mwingine aliyeonekana alikuwa ni nyani. Kwanza alionekana mmoja halafu akaonekana wa pili, wa tatu, nne, tano, sita, saba... sasa walikuwa wengine kuliko Dickson alivyoweza kuhesabu. Walikuwa wengi sana wakubwa na wadogo. Dickson alicheka sana, aliona hao nyani wanachekesha sana walivyokuwa wakiruka ruka na kupiga kelele.

Walikuwepo ndege wengi wazuri pia. Dereva Frank aliwaeleza mengi kuhusu wanyama na ndege waliowaona. Kila walivyoona mnyama mwingine Frank alisimamisha gari ili waweze kuwaangalia. Waliona pia pundamilia, twiga, kobe, mbuni na viboko.

Mama akasema, "sasa muda wa kula umefika". Dereva alisimamisha gari chini ya mti na wakatoa chakula mama alichokuwa amewafungia na wakaanza kula.

Walivyomaliza kula Dereva Frank akasema, "Kuna mnyama mmoja tu inabidi tumtafute. Ni mgumu kidogo kuonekana lakini"

Dickson alifikiria je huyu atakuwa ni mnyama gani na ikambidi aulize. Alishindwa hata kuanza kuuliza swali dereva Frank akasema, "Sshhhhh. Angalia pale". Alinyoosha kidole kuelekeza. Dickson hakuona kitu chochote. Lakini ghafla mnyama akasogea na kutoa mngurumo. Dickson aliogopa lakini akakumbuka kwamba yupo ndani ya gari na simba alikuwa hawezi kuingia. "Duh" alisema, "Simba mkubwa sana!" Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Dickson kuona simba.

Baada ya kumuona simba huyo ilikuwa ni muda wa kurudi nyumbani. Baba alikuwa amepiga picha nyingi za wanyama. Dickson alitaka picha ya yule simba aiweke ukutani ili kila siku aweze kuikumbuka safari yake nzuri.

Dickson anaenda safari

English

Dickson is a small boy and is 5 years old. Today Dickson is going on safari to see animals for the first time in his life. He is going with his mom and dad and his sister Lulu who is seven years old.

His mother woke up very early in the morning to prepare food for the safari and she also packed down drinking water. "Today it will be very hot so we will have to drink plenty of water", said his mom.

After having breakfast a big car came to pick them up. The drivers name was Frank and he was a good friend of dad.

All of them got into the car and began the safari. Before arriving where the animals were, Frank the driver stopped the car and opened the roof so that all of them could stand up and see better. "Very nice! Now we will see the animals very easily" said Dickson.

The first animal they saw was an elephant. The elephant was very big and Dickson got a bit scared so he had to hold his dad's hand. The elephant had very large ears and a long trunk.

Another animal they saw was a monkey. First there appeared one then the second, third, four, five, six, seven...now there were more than Dickson could count. There were big ones and small ones. Dickson laughed a lot, he found the monkeys very funny the way they jumped around and made noises.

There were many beautiful birds as well. Frank the driver told them many things about the animals and birds that they saw. Every time they saw another animal Frank stopped the car so that they could see them. They also saw zebras, giraffes, a tortoise, ostriches and hippos.

Then mom said, "Now it is time to have something to eat". The driver stopped the car under a tree and they took out the food that mom had prepared and they started eating.

When they finished eating Frank the driver said, "There is still one more animal we need to look for. But it's a bit hard to find."

Dickson thought what kind of animal this could be and he had to ask. He didn't even get to start asking his question when Frank the driver said, "Sshhhhh. Look over there." He pointed his finger to show. Dickson didn't see anything. But then suddenly the animal moved and roared. Dickson was very scared but he remembered that he was inside the car and the lion could not enter. "Wow" he said. "That's a very big lion!" It was the first time that Dickson had seen a lion.

After seeing the lion it was time to go back home. Dad had taken many pictures of the animals. Dickson wanted a picture of the lion to put up on the wall so that he could always remember his wonderful safari.